# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO NA MIFUGO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

**Mheshimiwa Spika,**

Naanza hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu, aliyetujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini mkubwa mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusiana na "Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo".

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuweka kipao mbele sekta ya Kilimo nchini, kwani ni dhahiri ya kwamba jitihada anazochukua Mheshimiwa Rais, za kuendeleza sekta hii ni kuona wananchi wa Zanzibar wanajiinua kuichumi na kujikomboa katika umasikini kwa kujiongezea kipato na kupata chakula cha uhakika na salama kwa lengo la kuwaondolea unyonge wananchi wetu wa visiwa vya Zanzibar.

Kadhalika, napenda kuwapongeza Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais kwa msaada mkubwa wanaompatia Mheshimiwa Rais, katika utekelezaji wa jukumu la uongozi wa nchi yetu. Namuomba mwenyezi Mungu awajaaliye afya njema na maisha marefu viongozi wetu ili tuzidi kuneemeka kwa uongozi wao bora.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis (Waziri wa Kilimo,

Umwagiliaji, Maliasili, na Mifugo), Katibu Mkuu, pamoja na jopo la watalaamu wao kwa mashirikiano waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Kadhalika, napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (AG) kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati. Ni dhahiri kuwa, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati yetu zililenga kuujenga zaidi mswada huu kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kupitia "Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo". Naomba kuwatambulisha Wajumbe hao pamoja na makatibu kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Dkt Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
10. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
11. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
12. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imeupitia kwa makini Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na

mambo mengine yanayohusiana na hayo, na kufanya baadhi ya marekebisho kwa nia ya kuwa fasaha na wenye tija zaidi. Marekebisho hayo yamehusisha makosa ya kiuandishi, kuingiza maneno yaliyokosekana ili kukamilisha maana iliyokusudiwa, kufutwa vifungu na kuandikwa upya, kuingiza vifungu vipya pamoja na kuingiza baadhi ya maneno ili kuleta upatanisho wa tafsiri baina ya nakala ya Kiswahili na ya Kiingereza ya Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 2 kimerekebiswa katika tafsiri ya neno **"aina"** kwa kuongezwa maneno yafuatayo mwishoni mwa tafsiri hiyo:

**(a) kuchukuliwa kama aina kuhusiana na kufaa kwake kwa kupandikizwa bila ya kubadilika;**

**(b) inafahamika kwa kuonesha sifa zitokanazo na matokeo ya kinasaba au mchanganyiko wa vinasaba; au**

**(c) kutofautishwa kutokana na sehemu ya mmea kwa kuonesha angalau moja ya sifa zilizotajwa."**

Marekebisho haya yaliyofanywa na Kamati yanalenga kuweka sawa mpangilio mzuri wa mswada huu ambapo kabla ya marekebisho vipengele hivyo viliweza kuleta sitofahamu kwa vile vimewekwa sehemu ambayo haikupaswa kuwekwa na kusababisha mgongano wa ufahamu. Mheshimiwa Spika, kwa kuliona hilo Kamati imeviweka vipengele hivyo sehemu stahiki na kuleta maana iliyokusudiwa kwa lengo la kuimarisha mswada wetu uwe na ufasaha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imependekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 12 kifungu kidogo cha (2)(c) kwa kuongezwa neno **"yanayokubalika"** baina ya neno **"utafiti"** na **"yasiyopungua"** ili kuhakikisha kuwa anapatikana Mkurugenzi Mkuu aliyebobea masuala ya utafiti hasa ikizingatiwa kuwa Taasisi hii inahusiana na mambo ya utafiti.

**Mheshimiwa Spika,**

Muingiliano wa majukumu katika kazi ni jambo ambalo linazorotesha ufanisi na utendaji kazi wa Taasisi husika na hatimae kuleta migogoro isiyokuwa ya lazima. Kamati imeliona hili wakati ilipopitia Mswada huu katika kifungu cha 27 kinachohusu kazi za Kamati ya Maadili ya Utafiti. Kupitia kifungu hiki yameanishwa majukumu mbalimbali ambayo yatafanywa na Kamati ya Maadili ya Utafiti ambapo baadhi ya majukumu hayo kupitia kifungu hiki yametia shaka utendaji kazi wake na kuonekana kama yanaingilia kazi za Bodi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 27(c) kimerekebiswa mwishoni mwa aya hiyo kwa kuondoa neno **"Bodi"** na kuweka badala yake neno **"Mkurugenzi Mkuu"** kwa lengo la kuzingatia majukumu na mipaka ya kazi katika Taasisi husika. Kamati imependekeza hivyo kwa kuwa Kamati ya Maadili ya Utafiti inateuliwa na Mkurugenzi Mkuu, hivyo, ni vyema taarifa za utekelezaji wa majukumu waliyopangiwa kuyawasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu kwa ajili ya kupata ridhaa yake na hatimae kuwasilishwa mbele ya Bodi ili kuepusha taarifa hiyo kuwasilishwa kwa Bodi bila ya ushauri wa Mkurugenzi Mkuu, jambo ambalo linaweza kuleta migogoro isiyokuwa ya lazima.

**Mheshimiwa Spika**

Kamati imependekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 27(e) kwa kuingizwa maneno **"mapitio ya"** baina ya neno **"ya"** na **"utafiti"** kwa kuwa jukumu lililowekwa awali moja kwa moja linahusiana na Bodi badala ya Kamati ya Maadili ya Utafiti.

**Mheshimwa Spika,**

Kwa kuepuka maamuzi binafsi ambayo huenda yakawa na maslahi binafsi katika Taasisi za Serikali na kuleta athari katika jamii, Kamati imeona ipo haja ya kukifanyia marekebisho kifungu cha 37 kwa kutoa nafasi zaidi kwa mtu ambaye hakuridhika na maamuzi yaliyofanywa na Taasisi hii kwa kuongeza hatua moja ya rufaa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na marekebisho yaliyopendekezwa mtu asiyeridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mkuu atakata rufaa kwa Bodi na endapo hakuridhika na maamuzi ya Bodi basi atakata rufaa kwa Waziri.

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambao tayari umeingizwa kwenye mfumo wa Baraza mtandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia, natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa taarifa yetu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu ili kuimarisha tafiti zetu za kilimo na mifugo na ziweze kuleta tija kwa wakulima na wafugaji wetu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

……………………………………………

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf,
Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.